# KAULI YA WAZIRI WA MAJI

## TAARIFA YA SERIKALI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MPANGO MAALUM WA KUBORESHA HUDUMA YA MAJISAFI NA MAJITAKA KATIKA JIJI LA DAR ES SALAAM

**Mheshimiwa Spika,** napenda kutoa tamko rasmi la Serikali kuhusu utekelezaji wa Mpango Maalum wa kuboresha huduma ya upatikanaji wa Majisafi na Uondoshaji wa Majitaka katika Jiji la Dar es Salaam kama Wizara yangu ilivyoahidi kufanya mara kwa mara.

**Mheshimiwa Spika,** Jiji la Dar es Salaam linao wakazi wanaokadiriwa kuwa milioni nne na laki tano. Mahitaji ya maji kwa ajili ya wakazi hao ni **lita 450 milioni kwa siku**. Wakati huo maji yanayozalishwa katika Mitambo ya Ruvu Chini, Ruvu Juu na Mtoni pamoja na Visima ni **lita Milioni 300 kwa siku**. Hii inamaanisha kuna upungufu wa **lita 150 milioni kwa siku**. Kutokana na hali hii ni maeneo machache ya Jiji yanayopata maji kwa muda wote. Mengine yanapata maji kwa mgao.

**Mheshimiwa Spika,** kwa wastani majitaka ni **asilimia 10** ya wakazi wa Jiji waliounganishwa kwenye mabomba ya kukusanya majitaka. Wengine waliobaki wanatumia vyoo vya shimo na matenki ya maji machafu (*Septic tanks*). Majitaka yanayokusanywa yanasafirishwa na kusafishwa katika mifumo ya mabwawa ya kusafisha majitaka.

**Mheshimiwa Spika,** ili kuondoa matatizo ya upungufu wa maji Jijini na kwenye maeneo yote yanayohudumiwa na DAWASA

pamoja na kuboresha uondoaji majitaka, mwaka 2006/2007 Serikali ilibuni na kuidhinisha Mpango Maalum wa Kuboresha Huduma ya Maji na Uondoaji wa Majitaka kwa Jiji la Dar es Salaam.

**Mheshimiwa Spika,** madhumuni ya mpango huo ni kuongeza wingi wa maji kutoka lita **milioni 300** kwa siku za sasa hadi lita **milioni 756** kwa siku ifikapo mwaka 2017. Hatua hii inaenda sambamba na kuboresha usambazaji wa maji, kupunguza upotevu wa maji yasiyolipiwa kutoka zaidi ya **asilimia 50** ya sasa hadi **asilimia 35** ifikapo Desemba, 2017 na kuboresha utendaji wa vyombo vinavyosimamia utoaji wa huduma katika maeneo hayo (*DAWASA* na *DAWASCO )* ili kuongeza uwezo wa utoaji wa huduma ya majisafi kwa wakazi wa jiji na maeneo ya Kibaha na Bagamoyo na kuongeza huduma ya wakazi wa Jiji wanaopata huduma ya uondoshaji wa majitaka kutoka **asilimia 10** ya sasa hadi asilimia **30** na kujenga Bwawa la Kidunda ifikapo Desemba 2017**.**

**Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa mpango huo unalenga kukabiliana na changamoto zinazolikabili Jiji la Dar es Salaam zikiwa ni pamoja na uchakavu wa miundombinu ya majisafi na majitaka, kupungua kwa maji katika Mto Ruvu, hasa wakati wa kiangazi, ongezeko kubwa la idadi ya watu la **asilimia 5.5** kwa mwaka ambalo ni kubwa ikilinganishwa na kiwango cha kitaifa cha ongezeko la watu mijini cha **asilimia 4.5** na ongezeko la shughuli za kiuchumi na kijamii lisiloendana na kasi ya uwekezaji katika uzalishaji na usambazaji maji katika Jiji la Dar es Salaam na Miji ya Kibaha na Bagamoyo.

**Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa Mpango Maalum wa Kuboresha Huduma ya Maji Jijini Dar es Salaam ambao unakadiriwa kugharimu **shilingi trillioni 1.088** ulianza rasmi mwezi Februari 2011, ambapo Serikali inaendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali kwa lengo la kukamilisha mpango huo. Hadi kufikia mwezi Machi, 2015, miradi inayotekelezwa ni kama ifuatavyo:-

**Upanuzi wa Mtambo wa Maji wa Ruvu Chini**

**Mheshimiwa Spika,** Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Kimarekani la *Millenium Challenge Co-operation* (MCC) imekamilisha upanuzi wa chanzo cha maji cha Ruvu Chini na upanuzi wa mtambo wa kusafisha maji (*Treatment Plant*). Kukamilika kwa upanuzi huo kumeongeza uzalishaji wa maji kutoka **lita milioni 180** hadi **lita milioni 270 kwa siku**. Mradi huo umegharimu jumla ya **Dola za Kimarekani milioni 36.8** sawa na **shilingi bilioni 66.24.** Kazi inayoendelea ni ulazaji bomba la kusafirisha maji kutoka Mtamboni kuja Jijini, iliyoanza mwezi Mei 2013 na hadi kufikia tarehe 31/12/2014 **kilomita 52.45** sawa na **asilimia 93** za bomba zimelazwa kati ya **kilomita 55.92**. Mradi huo umechelewa kukamilika kutokana na vikwazo na hasa miundombinu iliyopo katika njia ya bomba (nyaya za mawasiliano, nguzo za umeme na kesi zilizoko mahakamani). Mradi huo unatarajiwa kukamilika mwezi Juni 2015 kwa gharama ya **shilingi bilioni 120.2** kutoka Serikalini

Aidha Serikali inaendelea na ukarabati wa matenki ya kuhifadhia maji yaliyopo Chuo Kikuu cha Ardhi ambapo ukarabati huo umefikia **asilimia 89**.

**Upanuzi wa Mtambo wa Ruvu Juu**

**Mheshimiwa Spika,** Serikali kwa kutumia mkopo toka Serikali ya India inatekeleza mradi wa upanuzi wa mtambo wa Ruvu Juu, ulazaji wa bomba kuu la kutoka Mlandizi hadi Kimara, pamoja na ujenzi wa tanki jipya la Kibamba na kukarabati matenki ya maji Kimara.

- Mkandarasi wa kupanua chanzo cha maji eneo la Ruvu darajani ameanza kazi tarehe 15/02/2014 na kazi hii inatarajiwa kukamilika mwezi Agosti 2015. Hadi kufikia tarehe 28/02/2015 utekelezaji wa kazi hii umefikia asilimia 60. Kukamilika kwa upanuzi wa mtambo wa Ruvu Juu kutaongeza uwezo wa mtambo kuzalisha maji kutoka **lita milioni 82 kwa siku** hadi **lita milioni 196 kwa siku**. Kazi hii itagharimu **Dola za Kimarekani milioni 39** sawa na **shilingi bilioni 70.2**
- Mkandarasi wa Ujenzi wa Bomba Kuu kutoka Mlandizi hadi Kimara na ujenzi wa tenki jipya la maji la Kibamba ameanza kazi tarehe 11/03/2014 na kazi hiyo inatarajiwa kukamilika mwezi Septemba, 2015. Hadi kufikia tarehe 28/02/2015 utekelezaji umefikia asilimia 39. Gharama ya kazi hii ni **Dola za Kimarekani milioni 59** sawa na **shilingi bilioni 106.2**

## Uchimbaji wa Visima, Kimbiji na Mpera

**Mheshimiwa Spika**, Serikali pia inaendelea na kazi ya uchimbaji wa visima virefu katika maeneo ya Kimbiji/Mpera ambavyo vinatarajiwa kuzalisha **lita milioni 260 kwa siku**. Hadi kufikia tarehe 24/3/2015 mkandarasi amekamilisha visima vitatu, pia ameanza kuchimba kisima cha nne ambacho uchimbaji wake umefikia urefu wa **mita 400**. Aidha hivi sasa mkandarasi anaendelea na maandalizi ya kuchimba kisima cha tano. Kazi ya uchimbaji wa visima vyote 20 ilipangwa kukamilika tarehe 1/11/2014, hata hivyo kazi hiyo imechelewa kutokana na kuchelewa kuwasili kwa mabomba kutoka nje ya nchi (*Casing and Screens*). Kazi hiyo kwa sasa inatarajiwa kukamilika ifikapo Desemba 2015 na itagharimu **shilingi bilioni 18.48** kutoka Benki ya Dunia.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mradi wa kuchimba visima 20 vya kuzalisha maji, Serikali inatekeleza mradi wa visima nane vya uchunguzi wa Maji chini ya ardhi katika mwamba wa Kimbiji na Mpera. Hadi Kufikia Februari, 2015 mkandarasi amekamilisha uchimbaji wa visima sita na hivi sasa anakamilisha kisima cha saba. Mradi huu unagharimu **shilingi bilioni 7.54** zinazofadhiliwa na Serikali ya Norway.

**Ujenzi wa Bwawa la Kidunda**

**Mheshimiwa Spika,** Serikali pia inatekeleza mradi wa ujenzi wa **bwawa la Kidunda** ili kuhakikisha kwamba maji katika mto Ruvu yanakuwepo kipindi chote cha mwaka na **kuzalisha umeme** wa **megawati 20**. Mradi huu pia unahusu ujenzi wa **barabara** yenye urefu wa **kilometa 75** kutoka eneo la bwawa la Kidunda hadi Ngerengere na ujenzi wa **njia ya kusafirisha umeme** kutoka bwawa la Kidunda hadi Chalinze. Usanifu wa bwawa na barabara umekamilika na Serikali inaendelea na majadiliano na wadau ambao wameonesha nia ya kutekeleza mradi huu. Matarajio ni kuanza ujenzi katika mwaka wa fedha 2015/2016. Gharama ya mradi inatarajiwa kuwa **Dola za Kimarekani milioni 215** au **shilingi bilioni 387.**

**Mheshimiwa Spika,** ulipaji wa fidia kwa wananchi watakaohamishwa kupisha ujenzi wa bwawa la Kidunda na barabara ulifanyika kati ya mwezi Agosti na Septemba 2014. Idadi ya waliohusika na fidia ni **2,603** ambapo jumla ya shilingi **7,315,751,326.53** zilitumika kulipa fidia hiyo. Utayarishaji wa viwanja kwa ajili ya watakaoathirika na mradi umekamilika na zoezi la ugawaji linaendelea.

**Mheshimiwa Spika**, vilevile Serikali inaendelea na utaratibu wa ujenzi wa **Shule, Zahanati, Visima vya Maji, barabara** na miundombinu mingine katika vijiji vya Bwira Chini na Juu kwa ajili ya huduma za kijamii katika maeneo watakayohamishiwa wananchi

watakaoathirika na mradi. Utekelezaji wa kazi hizi utagharimu **shilingi bilioni 2.0.**

**Mradi wa Ukarabati na Upanuzi wa Mfumo wa Kusambaza Majisafi**

**Mheshimiwa Spika,** Serikali inaendelea kutekeleza mradi wa Ukarabati na Upanuzi wa Mfumo wa Kusambaza Majisafi kati ya Jiji la Dar es Salaam unaohusisha maeneo ya **Tegeta-Mpiji, Mpiji** hadi **Bagamoyo** na **Mbezi** hadi **Kiluvya**. Zabuni ya ujenzi imetangazwa na itawasilishwa tarehe 14 Aprili, 2015. Gharama ya kutekeleza mradi huo ni **Dola za Marekani milioni 140** au **shilingi bilioni 252**. Matarajio ni kuanza ujenzi wa mradi huu mwezi Juni 2015.

**Mheshimiwa Spika,** katika kuboresha hali ya upatikanaji maji katika Jiji zima la Dar es Salaam, Serikali imeanza utekelezaji wa mradi wa kulaza mabomba ya kusambaza maji katika jiji la Dar es Salaam, Kibaha na Bagamoyo katika maeneo yanayohudumiwa na DAWASA na DAWASCO **ambayo hayana mtandao wa mabomba kwa sasa**. Hivi sasa Serikali inaendelea na taratibu za kutafuta Mhandisi Mshauri wa kufanya kazi ya usanifu na uandaaji wa makabrasha ya zabuni. Hatua iliyofikiwa kwa sasa ni kuwa majadiliano ya Kimkataba na Kampuni iliyoshinda zabuni, *Ms. Consulting Engineers Salzgitter* ya Ujerumani yalifanyika tarehe 6/3/2015 na Mkataba utasainiwa hivi karibuni.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali pia, imesaini makubaliano ya awali (MoU) na mwekezaji juu ya kutafuta fedha na kutekeleza mradi wa kusafirisha maji kutoka Mpera na Kimbiji na kuyasambaza kwa wananchi katika maeneo ya **Mkuranga, Chamazi, Msongola, Chanika, Gongolamboto, Pugu, Kitunda, Uwanja wa Ndege, Kinyerezi, Vituka, Kiwalani na Vingunguti**. Mwekezaji anakamilisha taarifa ya awali (*Feasibility report)* ambayo itawasilishwa mapema mwezi Aprili 2015. Matarajio ni kukamilisha majadiliano na kuanza utekelezaji wa mradi mwaka wa fedha 2015/2016.

**Mradi wa Uboreshaji Mfumo wa Uondoshaji Majitaka**

**Mheshimiwa spika**, Serikali inatekeleza mradi wa kuondosha majitaka katika Jiji la Dar es salaam ili kuongeza eneo linalohudumiwa na kutoka **asilimia 10** ya wakazi wanaohudumiwa kwa sasa kufikia **asilimia 30** ifikapo 2017. Utaratibu wa kupata mshauri atakayesanifu mradi huu umekamilika na matarajio ni kusaini mkataba mwezi Aprili 2015.

Aidha, Serikali imeendelea kuongea na washirika wa maendeleo walionyesha nia ya kutoa fedha kwa ajili ya mradi huu mkubwa.

**Mheshimiwa Spika**, mnamo tarehe 5 Machi 2015 Serikali ya Tanzania ilisaini makubaliano ya kisera (*Policy Dialogue)* na Serikali ya Korea ambapo Serikali ya Korea imekubali kutoa **Dola za Kimarekani 89 milioni** au **shilingi bilioni 160.2** kugharamia utekelezaji wa mradi huu. Makubaliano ya awali ya mpango wa

utekelezaji wa mkataba wa kifedha *(Framework Agreement)* yalisainiwa tarehe 25 Machi 2015. Matarajio ni kuanza kutekeleza mradi mapema mwaka 2016. Kazi zitakazofanyika chini ya mradi huu ni pamoja na upanuzi wa mfumo wa majitaka katika maeneo ya **katikati ya jiji, ujenzi wa mfumo mpya Ilala, Magomeni** hadi **Ubungo, Sinza, Kinondoni, Mwananyamala, Oysterbay, Masaki, Msasani, Kawe, Mbezi Beach, Kurasini, Keko, Chang'ombe** na **Temeke .** Mradi huu pia utahusu ujenzi wa mitambo mitatu ya kisasa ya kusafisha majitaka itakayojengwa katika maeneo ya **Jangwani, Kurasini** na **Mbezi Beach**.

**Mradi wa Visima katika maeneo yasiyo na mtandao**

**Mheshimiwa Spika,** ili Kuhakikisha wananchi wasiopata huduma ya maji kutoka mtandao wa maji wa DAWASCO wanapata maji, Serikali inatekeleza mradi wa visima vidogo maeneo mbalimbali ya jiji. Hadi sasa visima **48** vimechimbwa na visima 23 vinatoa huduma. Maeneo yaliyonufaika hadi sasa ni **Mavurunza A, Kilungule A na B, King'ongo I, King'ongo III, Sandali. Mpogo, Mwemberadu, Mburahati, Kipunguni, FFU Ukonga, Mongo la Ndege, Segerea, Chanika na Yombo, Saranga I na Saranga II), Chang'ombe A, Unubini, Chang'ombe Toroli Keko Magurumbasi** na **Keko Mwanga**. Utekelezaji wa mradi huu utaendelea mpaka baada ya ujenzi wa miradi ya kuboresha upatikanaji wa maji katika maeneo yote itakapokuwa imekamilika.

**Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza Mpango huu kumekuwa na changamoto mbalimbali. Changamoto kubwa zimekuwa ni upatikanaji wa maeneo ya kujenga miradi na upatikanaji wa fedha. Ninaushukuru uongozi wa mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Morogoro kwa ushirikiano na msaada wao mkubwa walioutoa katika kupata ufumbuzi wa changamoto zilizojitokeza.

**Mheshimiwa Spika,** miradi inayotekelezwa ili kuboresha hali ya upatikanaji maji kwa Jijii la Dar es Salaam ni miradi mikubwa inayohitaji fedha nyingi na muda ili kuitekeleza, tunawaomba Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla wawe na subira katika kipindi hiki ambacho Serikali inatekeleza miradi hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali sikivu ya **Chama cha Mapinduzi** imekuwa ikitenga fedha nyingi kwa Jiji la Dar es Salaam ikilinganishwa na maeneo mengine kwa mfano mwaka 2013/2014 bajeti nzima ya Serikali kwa ajili ya miradi ya Maendeleo kwa Sekta ya Maji ilikuwa **shilingi bilioni 553.2** wakati Dar es Salaam zilitengwa **shilingi bilioni 101.6** sawa na **asilimia 18.4** ya bajeti nzima na mwaka 2014/2015 bajeti nzima ni **shilingi bilioni 488.9** wakati Dar es Salaam zimetengwa **shilingi bilioni 68** sawa na **asilimia 14** ya bajeti nzima.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge na wananchi kuwa kuanzia mwezi Juni hadi Septemba, 2015, hali ya upatikanaji wa maji katika jiji la Dar es Salaam,

maeneo ya Kibaha na Bagamoyo yanayohudumiwa na DAWASA na DAWASCO itakuwa imeboreka kwa kiwango cha kuridhisha sana.

**Mheshimiwa Spika**, nakushukuru wewe na Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha.

PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE (MB)

**WAZIRI WA MAJI**

**Dodoma, 31 Machi 2015.**

Formatted: Centered